JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO
YA UFUNDI STADI

# CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI WILAYA YA BUTIAMA

## MAHITAJI MUHIMU YA MWANACHUO

1. Unatakiwa kununua vifaa na mahitaji yafuatayo kwa matumizi yako ukiwa chuoni;-

**A. Sare ya chuo**

(i) Mashati mawili meupe ya mikono mfupi kitambaa cha tetroni.

(ii) Suruali mbili za rangi ya bluu iliyokoza (dark blue) zinapatikana chuoni

(iii) Jozi ya **viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi** vitakavyovaliwa wakati wa mafunzo ya nadharia madarasani.

(iv) Ovaroli moja ya rangi ya bluu iliyokoza (dark blue) inapatikana chuoni

(v) Soksi ndefu Jozi mbili za rangi **nyeupe**

(vi) Sweta ya rangi ya bluu iliyokoza (dark blue) inapatikana chuoni

**B. Vifaa Vingine**

(i) Madaftari makubwa saba (7) ya **3Q**

(ii) Seti ya vifaa vya hesabu (Mathematical set).

(iii) Kalamu za wino na penseli (2B na HB) za kutosha

(vi) Rimu moja ya karatasi za A4 aina ya **Double A** au **Mapacha** (*itakabidhiwa ofisini*).

2. Unatakiwa kuja na kiasi cha fedha za kulipia mahitaji yaliyoorodheshwa hapa chini. Ufikapo chuoni, utapewa namba ya malipo ya serikali (Control number) na utahitajika kulipia na kuwasilisha stakabadhi ya malipo kwenye ofisi ya mhasibu isipokuwa namba (vi) ambayo italipwa baada ya kukamilisha usajili na control namba itatolewa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF)

## JEDWALI A (Control number itatolewa chuoni isipokuwa namba vi)

| Na | Mchanganuo wa Malipo | KIASI (TSHS) | |
|---|---|---|---|
| | | **AWAMU YA I** | **AWAMU YA II** |
| i | Ada ya mafunzo (KUTWA) | 30,000/= | 30,000/= |
| ii | Ada ya mafunzo (BWENI) | 60,000/= | 60,000/= |
| iii | Fedha ya Uchakavu | 10,000/= | |
| iv | Fedha ya Vifaa vya Michezo | 10,000/= | |
| v | Fedha ya Vifaa vya Usafi | 10,000/= | |
| vi | Bima ya Afya (NHIF) | 50,400/= | |
| **JEDWALI B ( fedha hii ilipwe chuoni siku utakapowasili**) | | | |
| vii | Suruali mbili rangi ya dark blue@20,000 | 40,000/= | |
| viii | T-Shirt ya VETA | 16,000/= | |
| xi | Ovaroli moja rangi ya dark blue | 30,000/= | |
| x | Kitambulisho (ID) | 5,000/= | |
| xi | Nembo ya VETA (Emblem) | 5,000/= | |
| xii | Sweta la dark blue lenye V-shape | 16,000/= | |
| | **JUMLA(KUTWA)** | **222,400/=** | **30,000/=** |
| | **JUMLA(BWENI)** | **252,400/=** | **60,000/=** |

3. Wanafunzi wa Bweni wanatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo kwa matumizi wakiwa chuoni;

    (i) Vyombo vya chakula - sahani, bakuli, kikombe na kijiko.

    (ii) Shuka mbili, blanketi, chandarua na nguo nyingine za kubadilisha inapohitajika.

    (iii) Ndoo na beseni kwa ajili kuchotea maji na kuogea, pamoja na vifaa vingine vya usafi binafsi kama sabuni, mafuta ya kujipaka,miswaki na dawa za meno.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI WILAYA YA BUTIAMA

# SHERIA ZA CHUO KWA WANAFUNZI WA KUTWA NA BWENI

**ILI KUFANIKISHA MAFUNZO YA AWALI YA UFUNDI KILA MWANAFUNZI ANATAKIWA KUFUATA SHERIA ZIFUATAZO:**

1. **MAHUDHURIO:**

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi. Hii ina maana ifikapo saa 1:30 wanafunzi wote wawe wameshafika chuoni. **ADHABU KALI ITATOLEWA KWA WACHELEWAJI**.

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali, au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kuruhusiwa na Mwalimu wa zamu kupitia kwa mwalimu wa darasa.

(c) Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba, kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.

(d) Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi atakosa sifa za kufanya mitihani ya Taifa.

2. **MAVAZI:**

(a) Sare ya chuo ni suruali ya dark blue na shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya VETA. Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Wakati wote shati liwe limechomekewa.

(b) Ovaroli livaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.

(c) Viatu vyenye visigino virefu na kanda mbili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

3. **USAFI WA MWILI:**

(a) Hairuhusiwi kuvaa heleni, pete, bangili na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo. Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

**(b)** **NYWELE KWA WAVULANA:**

i. Zikatwe ziwe fupi sana, KIPARA hakiruhusiwi kabisa.
ii. Ndevu haziruhusiwi na ndevu aina zote haziruhusiwi mustachi/sharubu.

**(c)** **NYWELE KWA WASICHANA:**

(i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma.

(ii) **kucha zisifugwe kabisa wala kupaka rangi.**

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**

(a) Vitendo vyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali za chuo au mwanafunzi mwenzake, basi atafukuzwa chuo mara moja.
(b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa na ukakinunue kifaa chenyewe au ulete badala ya ulichokipoteza.
(c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.
(d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

Ugomvi, kupigana au kushambuliana ni makosa ya jinai. Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo atafukuzwa chuoni na kukabidhiwa kwenye vyombo vya dola.

6. **ULEVI:**

Iwapo itabainika mwanafunzi analewa au kuonekana katika sehemu za vileo, anavuta bangi au madawa ya kulevya adhabu yake ni kufukuzwa chuo mara moja.

7. **MAPENZI:**

(a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi/mwalimu na mwanafunzi hairuhusiwi kabisa.
(b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi watumishi bila ya kibali au ruhusa.

8. **MIGOMO:**

Migomo ni marufuku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika. Mwanafunzi atakayeshawishi au kusababisha migomo atafukuzwa chuoni mara moja.

9. **LUGHA:**

Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.

10. **KUBADILISHA JINA:**

Jina lisibadilishwe mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na ajulishwe Mkuu wa Chuo mara moja.

11. **MATUMIZI YA SIMU WAKATI WA MAFUNZO**

Ni marufuku kuwasha/kutumia simu za mkononi wakati wote wa vipindi.

## SHERIA ZA NYONGEZA KWA WANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya Chuo siku zifuatazo tu:

(i) Jumapili kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni
(ii) Jumamosi kuanzia saa 7:30 mchana hadi saa 12.00 jioni
**(iii) Majina yaandikwe kwenye kitabu cha kutoka na kuingia. Mhusika aandike muda wa kutoka na kusaini arudipo.**

13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na kitambulisho cha Chuo na sare ya chuo na atajiandikisha lango kuu. Mwanafunzi atakayeonekana nje ya maeneo ya Chuo bila kitambulisho na sare ya chuo atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya kulala bwenini au kufukuzwa chuoni

14. Mwanachuo atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya Chuo bila kibali atasimamishwa masomo.

15. Hairuhusiwi kupikia chakula bwenini, na atakayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.

16 (a) Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.

(b) Hairuhusiwi **KABISA** kwa mwanachuo kuingia katika eneo wanamoishi wafanyakazi wa Chuo bila ruhusa au kibali.

17 Hairuhusiwi kupeleka chakula bwenini. Endapo kuna mgonjwa, ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.

18 Taa za madarasani na mabwenini zizimwe ikiwa hazitumiwi na usiku zizimwe saa 4:00 za usiku.

19. Hakuna ruhusa kumkaribisha au mgeni kulala bwenini, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni au ndugu siku ya masomo, ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.

- Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.
- Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.

20. Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya Chuo.

21. Ruhusa ya kulala nje ya mipaka ya Chuo itatolewa na Ofisi ya Mkuu wa Chuo tu.

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY**

**BUTIAMA DISTRICT VOCATIONAL TRAINING CENTRE**

**THE MEDICAL OFFICER**

**Government Hospital/ Dispensary**

………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF ……………………………………….**

Please examine the above named trainee to certify his/her fitness to undergo training and subsequently work as/an artisan
in ………………………………………………………….

(i) Eyesight …………………………………………...
(ii) Hearing ……………………………………………
(iii) Asthma …………………………………………….
(iv) Other serious diseases……………….................

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I have examined the above named trainee and consider that he/she is physically fit/ unfit for training as above.

Date **………………** Designation……………………………………………………………

Signature & Official Stamp **……………………**

# CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI WILAYA YA BUTIAMA

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi **…………………………………………………………………………** ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo.

Sahihi **……………………………………..** Tarehe **………………………….**

**b) MZAZI/MLEZI/MDHAMINI**

Mimi **……………………………………………………………………………….....**

Mahusiano ………………………………………………………………………….…

S. L. P. …………………………… Simu ……………………………..

Kijiji/Mtaa…………………………………… Kata ……………………………
Wilaya ……………………………………… Mkoa ……………………………

Ninathibitisha kuwa ninamdhamini mwanachuo aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (Ada na michango mingine) pamoja na nauli wakati wote wa kwenda na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo ya awali.

Sahihi **……………………………………..** Tarehe **………………………….**